

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 022 2112065-7  
Fax No. +255 022 2112538  
E-mail: [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 9133,  
DAR ES SALAAM

**SPIKA WA BUNGE MHE JOB NDUGAI (MB) AELEKEZA VIKAO VYOTE  
VYA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUFANYIKIA MJINI  
DODOMA KUANZA TAREHE 22 AGOSTI, 2016.**

---

Spika wa Bunge Mhe. Job Ndugai (Mb) ameagiza Mikutano yote ya Kamati za Kudumu za Bunge inayotarajiwa kuanza tarehe 22 Agosti, 2016 mpaka 4 Septemba, 2016 kufanyika Mjini Dodoma kabla ya Mkutano wa Nne wa Bunge unaotarajiwa kuanza tarehe 6 Septemba, 2016.

Maagizo haya ya Mhe. Spika ukiwa ni utaratibu endelevu kwa vikao vingine vya kamati za Bunge vitakavyofuatia ameyatoa katika waraka wake Na. 6/2016 kwa Waheshimiwa kwa kuzingatia Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inayosema: **“Mikutano ya kawaida ya Kamati za Bunge za Kudumu itafanyika Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar”** na kwa kuzingatia maagizo ya Serikali kuchagiza uhamiaji wa Makao Makuu mjini Dodoma kwa Mawaziri na Watendaji wa Serikali ambao kimsingi ndio wahusika Wakuu wanaokutana na Kamati za Kudumu za Bunge.

Katika waraka wake huo, Mhe. Spika amesema Bunge ni Mhimili ambao tayari ulikwishatekeleza kwa vitendo kuhamia Dodoma kwa baadhi ya Mikutano yake kufanyika Makao Makuu tangu Oktoba, 1974 na baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 tulihamishia Mikutano yote ya Bunge Dodoma. Hata hivyo, Vikao vya Kamati ambavyo hufanyika kabla ya Mikutano ya Bunge viliendelea kuwa Dar es Salaam kwa kuwa vilihitaji uratibu wa karibu na Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ikiendesha shughuli zake Dar es Salaam.

Kwa kuwa Mhimili wa Bunge umekwishahamia Dodoma ila baadhi ya huduma za utawala na watumishi waliendelea kuwa Dar es Salaam kwa mawasiliano na uratibu na Serikali, kwa sasa nao watahamia Dodoma.

Mhe. Ndugai amesema hivi sasa Bunge na Serikali vinaelekea katika kuwa mahali pamoja kwa maana mji ambao Bunge linakutana ndio hapo hapo yanapokuwa Makao Makuu ya Serikali, na kusisitiza kuwa huko mbele itafanyika tathmini iwapo mfumo wa sasa uliopo wa Mikutano ya Bunge kutanguliwa na Vikao vya Kamati ndio unaofaa au kuwa na mfumo bora zaidi wa kuunganisha Vikao vya Kamati na Bunge kwa pamoja kama ilivyo kwa nchi nyingine katika mifumo yao ya Bunge pale ambapo Bunge na Serikali wako katika Mji mmoja.

Kufuatia maagizo haya ya Mhe. Spika, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na watendaji/ wahusika katika vikao vya kamati wanatakiwa kujipanga kukutana Dodoma kwa kuzingatia ratiba za kila kamati zitakazotolewa hapo baadae.

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
**Dar es Salaam**

29 Julai, 2016.